



Kwa ajili ya kupambana na maenezi ya ugonjwa wa COVID-19 Michigan, Gavana Whitmer alitia saina agizo la mtendaji la “Baki Nyumbani, Baki Salama”. Angalau hadi tarehe 30 za mwezi wa nne, biashara na oparesheni zote za Michigan lazima zifungwe, oparesheni zinazohitaji mtu binafsi kuwepo eneo husika na ambazo sio za lazima kwa maendeleo au kulinda maisha zifungwe, na watu wote wa Michigan lazima wabaki majumbani mwao isipokuwa wale ambao ni miongoni mwa miundombinu muhimu ya nguvukazi, wanaofanya kazi zinazoshiriki shughuli za nje, au wanaofanya kazi ambazo ni muhimu kwa afya na usalama wao na familia zao, kama kwenda hospitalini au kwenda madukani.

UNAWWEZA:

- Kwenda dukani au kupokea chakula cha kununua nje.
- Kwenda kwenye duka la dawa kuchukua dawa inayohitajika.
- Kwenda matembezini, kupanda mlima, kukimbia, kuendesha baiskeli.
- Kwenda hospitalini au kushughulikia huduma yoyote muhimu ya matibabu au kuhifadhi afya yako au afya ya mpendwa wako.
- Kujaza gari lako mafuta
- Kurudi nyumbani iwapo umetoka safarini nje ya Michigan
- Kurudi nyumbani ambako unaishi mbali na Michigan
- Kuwapeleka matembezini wanyama wa majumbani na kuwapeleka kwa daktari wa mifugo kama watahitaji huduma

HUTAWWEZA:

- Kutoka nyumbani isipokuwa wewe ni mfanyakazi wa miundombinu muhimu au unahitajika kuendeleza shughuli za msingi za biashara
- Kushiriki mikutano ya hadhara ya aina yoyote
- Kumtembelea mtu yeyote hospitalini, kwenye nyumba za uuguzi, au vifaa vingine vya makazi (isipokuwa wachache watakaopewa ruhusa)
- Kwenda kwenye maduka makubwa au kwenye migahawa

BIASHARA AMBAZO ZITABAKI KUFUNGULIWA KWA WAFANYAKAZI WANAOHITAJIKA KUENDA KAZINI LAZIMA ZICHUKUE HATUA KALI ILI KUPUNGUZA KUENEA KWA UGONJWA

- Wakuze kazi zinazoweza kufanyika mbali na eneo la kazi kwa kiwango kamili iwezekanavyo
- Wapunguze idadi ya wafanyakazi waliopo kazini
- Wahakikishe mfanyakazi yuko angalau hatua sita mbali na mwenzake kwa kiwango kinachowezekana na kuwawezesha wanajamii kuwa mbali na wateja ambao wanaosubiri huduma kwenye mistari
- Kufuata njia nyingine zozote za kukaa mbali zinazoshauriwa na kitengo cha Kudhibiti Magonjwa
- Ni lazima maduka makubwa yapunguze idadi ya watu watakaokuwa dukani kwa wakati mmoja ili kusiwe na zaidi ya watu 4 kwa kila futi 1,000 za mraba ya nafasi ya kupitia wateja.
- Ni lazima maduka madogo yapunguze idadi ya wateja hadi asilimia ishirini na tano (pamoja na wafanyakazi) chini ya misimbo au nambari za moto.

- Ili kudhibiti kuingia, ni lazima maduka yaweke mistari iliyo na alama kwa wateja ili kuwasaidia wasimame umbali wa angalau futi sita kutoka kwa wenzao wanapongojea kuingia.
- Ni lazima maduka makubwa yafunge sehemu za duka ambazo zimetengwa kwa kuuza bidhaa za kuweka zulia, kutengeneza sakafu, vituo vya bustani, miche ya kupanda au sehemu ya kuuza rangi.

Habari zinazohusu virusi zinabadilika kwa uharaka sana hivyo habari mpya zitapatikana **[Michigan.gov/Coronavirus](https://www.michigan.gov/Coronavirus) na **[CDC.gov/Coronavirus](https://www.cdc.gov/Coronavirus).****

Kwa walio na maswali kuhusu hatua ya Michigan ya kuwahifadhi wanajamii kutokana na uenezi wa virusi vya corona, tafadhali piga simu ya COVID-19 kwa nambari 1-888-535-6136 kati ya 8 am- 5 am kila siku.